# Jarida la UQAB

Toleo 43 - Dhul hijjah 1441 H / Agust 2020 M




# Ugumba wa kuweka uaminifu wetu kwa Umoja wa Mataifa

uqab.or.ke
uqab_htk
UQAB-Magazine-1911964012162253



# Ugumba wa kuweka uaminifu wetu kwa Umoja wa Mataifa

**Srebrenica-**Miaka 25 imepita sasa ambapo zaidi ya wavula na wanaume wa Kiislamu 8,000 kutoka Srebrenica, mji mdogo, ulio na wakaazi wengi mno, nchini Bosnia, waliuwawa katika yale yanayo onekana sasa kuwa ndio mauwaji mabaya zaidi katika ardhi ya Ulaya tangu Vita vya Pili vya Dunia.
Kuanguka kwa eneo la Waholanzi ambalo lilikuwa limetangazwa kuwa mojawapo ya "maeneo salama" sita yaliyopewa ulinzi na Dutchbat, kikosi cha Uholanzi kilicho pelekwa kule kama Jeshi la Ulinzi na Umoja wa Mataifa, ilikuwa ndio sura ya mwisho katika vita vya miaka minne katika ile iliyokuwa Yugoslavia.

Idadi ya watu eneo hilo iliongezeka kwa ghafla huku wakimbizi waliokuwa wametawanyika baada ya kimbunga cha ghasia katika kutafuta ruwaza ya Milosevic ya "Serbia Tukufu." Wakitafuta usalama kutokana na mashambulizi, mauwaji, kufurushwa kwa lazima, kambi za msongamano, mateso na dhulma za kimapenzi dhidi ya wanawake takriban 50,000 ambao walibakwa kwa mpangilio, kufanywa watumwa na kutungwa mimba kwa nguvu.

Mauwaji ya Srebrenica yanaonekana kuwa ndicho kitendo kibaya zaidi cha kuogofya wakati wa vita hivyo, haswa kwa kuwa yalifanyika chini ya jicho angalizi la Umoja wa Mataifa, ambao ulicheza sehemu katika kuwapokonya silaha wanaume wa Kiislamu kufuatia matakwa ya Serbia, ili kuunda "eneo-salama", waliwasaidia Waserbia katika kuwatenganisha wanaume na wanawake katika siku ya mauwaji hayo na wakawaruhusu wanaume waliokuwa wametafuta hifadhi katika uwanja wa Waholanzi kutolewa na majeshi ya Serbia wakijua fika hatma yao itakuwa ni ipi.Kwamba Umoja wa Mataifa ulifeli vibaya mno kulinda maisha ya wanaume na wavulana 8,000 na kwamba walisalia kuwa watu waliosimama kando, huku wanawake wakidhulumiwa kwa kiasi kikubwa ndio ukweli. Ilhali tungali tunaona kwamba kila kadhia mpya inayoibuka ndani ya Ummah, Umoja wa Mataifa bado huonekana kama shirika lenye uwezo wa kutatua tatizo. Kufeli kumoja huenda kusitosheleze kuukinaisha Ummah kwamba Umoja wa Mataifa kamwe hauwezi kutimiza dori yake, lakini, ili kupima fikra kama hiyo, hebu tutathmini msururu wa rekodi ya Umoja wa Mataifa kuhusiana na Ummah huu. Hivyo kando na kufeli kwao katika kuwalinda Waislamu nchini Bosnia je, wamefanya lipi la maana katika kuwalinda Waislamu katika historia yake yote?



**Palestine-**Tangu uvamizi wa Palestina, Wapelestina wamekuwa wakipigana dhidi ya kile ambacho mchunguzi wa Umoja wa Mataifa aliwahi kukitaja kama "sifa zisizokubalika za ukoloni, ubaguzi wa rangi na mauwaji ya kimbari". (Richard Falk)

**Leo licha ya maazimio ya Umoja wa Mataifa,** "Israel" **imeongeza udhibiti wake wa maeneo ya Palestina. Imelazimisha vikwanzo vyenye kulemaza juu ya Gaza na ingali inaendelea na ujenzi wake wa makao yasio halali juu ya ardhi zilizo kaliwa.**
Historia imetufunza kwamba "Israel" hata mara moja haijawahi kutii azimio lolote la Umoja wa Mataifa ambalo haliko kwa manufaa yake kikamilifu. Vilevile usaidizi wa Amerika kwa "Israel" umekuwa dhahiri zaidi ikipinga azimio lolote ambalo halihifadhi maslahi ya umbile la Kiyahudi,

hata vikwazo vya kinyama juu ya ukanda wa Gaza, kujenga makao yasiyo halali juu ya ardhi ya Palestina katika Ukingo wa Magharibi, au kuwaweka kuzuizini watoto wa Palestina kwa ajili ya uchunguzi huku ikiwadhalilisha wafungwa kwa rai na maandamano.

**Iraq**-Uvamizi wa Amerika kwa Iraq mnamo 2003, ambao ulikuwa si halali na bila ya idhini ya Baraza la Usalama, waziwazi unamulika ukweli kwamba uwezo wa Umoja wa Mataifa una kikomo katika kudhibiti vitendo vya dola kuu.

Waundaji wa Baraza la Usalama walibuni kura ya turufu ili yeyote katika wanachama watano wa kudumu aweze kukataa azimio la Baraza hilo. Hivyo ikiwa "nguvu" za ulimwengu zinataka kuvamia, hakuna lolote la kuzizuia.

Katika kesi ya uvamizi wa Iraq, Amerika hata haikupiga kura ya turufu kwa azimio, bali ilitafuta idhini ambayo haikuipata.

Umoja wa Mataifa, ulipaswa kujibu kwa kuihami Iraq dhidi ya matumizi ya nguvu yasiyo halali. Badala yake ulisalia tasa huku uvamizi huo ukithibitisha kuwa ni janga la kibinadamu kwa potea kwa maisha zaidi ya 400,000.




**Kashmir**-Makabiliano yanayo endelea katika eneo la Kashmir inayozozaniwa yamekuwa mojawapo ya majanga makubwa zaidi ya haki za kibinadamu katika historia, yakidhihirishwa na mauaji ya Wanton, ubakaji, kuwekwa kizuizini kwa viongozi na wanaharakati, mateso na kupotezwa kwa Wakashmir, yote haya yanafanyika huku kukiwa na maazimio mingi ya Umoja wa Mataifa juu ya kadhia hii.

Mnamo 1948, Amerika na Uingereza ziliahidi kuwa mustakbali wa Kashmir ni lazima uamuliwe na mapenzi ya watu wake. Matakwa yao ni lazima yaamuliwe kupitia kura ya maamuzi chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa. Amerika ndio iliyokuwa mdhamini mkuu wa azimio nambari 47 lililotabanniwa na Baraza la Usalama mnamo Aprili 21, 1948 na ambalo liliundwa juu ya msingi huo usiopingika.

Badala yake Umoja wa Mataifa imetazama kama shabiki huku India ikiyachana maazimio yake juu ya Kashmir na kipeke yake ikifutilia mbali Kifungu 370 na 35-A cha kumaliza hadhi maalum ya Kashmir. India imeanzisha msako mkubwa katika Kashmir iliyo kaliwa. Amri ya kutotoka nje usiku iliyo lazimishwa na majeshi ya India bado ingalipo. Kuna uhaba mkubwa wa dawa na chakula bondeni humo. Watu wengi wanakabiliwa na baa la njaa. Wagonjwa wamenyima matibabu. Majeshi vamizi ya India yanawapiga na kuwadhalilisha watu wale wote wanaosubutu kutoka nje na yale yote ambayo Umoja wa Mataifa na dola za ulimwengu ziko tayari kufanya ni kutazama kimya kimya huku majeshi ya India yakitekeleza mauaji haya.
**Yemen**-Muungano unao ongozwa na Saudia, ambao unasaidiwa kijeshi na kisiasa wa Imarati, Amerika, Uingereza, Ufaransa,

"Israel", Misri, Bahrain, na mataifa mengine, ulianzisha vita juu ya Yemen mnamo 2015 ambavyo vimetajwa na Umoja wa Mataifa wenyewe kama "mojawapo ya maafa mabaya zaidi ya kibinadamu katika historia ya zama hizi." Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, kufikia mwisho wa 2019, mapigano hayo yatakuwa yamechukua maisha ya watu 102,000. Zaidi ya hayo vita hivyo vimewaacha mamilioni bila ya makao, huku milioni 19 wakiteseka kutokana na umasikini na hatari ya baa la njaa.

Umoja wa Mataifa umefanya nini?

Hawajawataja majina wale ambao wanahusika waziwazi na maafa haya, na kihakika waliitisha suluhisho la kisiasa (mnamo 2016) ambalo litahifadhi kwa njia isiyo ya moja kwa moja maslahi ya Saudi Arabia huku likiitambua serikali mpya iliyoundwa mjini Sanaa. Sio Umoja wa Mataifa wala jamii ya kimataifa iliyotaja kuwa Saudi Arabia na Imarati ndizo vyanzo vya moja kwa moja vya maafa haya kwa kiwango mkubwa, kupitia usaidizi wa Amerika, "Israel", Uingereza, na Ufaransa.
Vilevile tangu kuzuka kwa vita nchini Yemen, imepokea fedha zaidi ya dolari bilioni 8 kutoka kwa makongamano ya wafadhili kwa ajili ya Yemen, huku watu wa Yemen wakiendelea kuteseka kutokana na umasikini, njaa na maradhi.
**Rohingya**-Katika ripoti moja iliyo chapishwa mwaka mmoja uliopita ikiongozwa na aliyekuwa Waziri wa Kigeni wa Guatemala, Gert Rosenthal inatamatisha: katika upuzi wa kughadhabisha wa kidiplomasia wa taasisi, ambao mfumo mzima wa Umoja wa Mataifa




umekuwa ndani yake ni "utasa wa kufanya kazi inavyostahili pamoja na mamlaka za Myanmar, ili kugeuza mitindo miovu katika nyanja za haki za kibinadamu, na kumakinisha mitindo mizuri katika nyanja nyenginezo."
Kwa lugha nyepesi, Umoja wa Mataifa haukufanya lolote kuzuia Myanmar kutokana na kutekeleza mauwaji ya halaiki ya Rohingya wa jimbo la Rakhine.Ghasia ambazo zilitumiwa ni za kushtua, hata hivyo hazikutarajiwa. Tafiti zimefafanua kwamba mapema tangu 2015 kampeni ya mauwaji ya halaiki tayari ilikuwa imeanza. Kwa viashiria vya wazi kwamba janga linakuja, kwa nini ulimwengu ulishindwa kuwalinda Rohinya? Hususan tunapogundua kuwa Umoja wa Mataifa uliidhinisha Jukumu la Kulinda (R2P) mnamo 2015, linalo wajibisha jamii ya kimataifa kulinda raia kutokana na mauwaji ya halaiki pindi serikali zao zinapokuwa "haziko tayari au haziwezi" kuwaweka katika usalama. R2P ilikubaliwa kutokana na hatia jumla juu ya uchinjaji wa halaiki wa raia nchini Rwanda na Bosnia na kuahidi enzi mpya ya majibu ya "hapo kwa hapo na makali" kwa mauwaji.

Katika kulipata lengo hili, onyo la mapema la juhudi za kutambua viashiria vya mauwaji ya halaiki likawa ndio angazo la watekelezaji wa kimataifa pamoja na wa dola. Hadi sasa yote yaliyofanya ni kunakili ubakaji mkubwa wa magenge, mauaji – ikiwemo ya watoto wachanga na wadogo – kipigo cha kikatili na upotezaji watu unaofanywa na majeshi ya dola ya Myanmar. Na kuwataja Rohingya kuwa "watu wanaoteswa zaidi duniani."



**Syria**-Umoja wa Mataifa umeeleza kuwa kwa uchache watu 250,000 wameuwawa kati ya 2012 na 2017. Lakini, shirika hilo lilisitisha kujadidisha tarakimu zake mnamo 2015. Shirika la Kuchunga Haki za Kibinadamu la Syria linakiweka kiwango cha vifo kuwa zaidi ya 321,000, huku tathmini nyengine ikieleza kuwa mzozo huo umesababisha vifo 470,000, ima kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja.

Watu milioni tano – wengi wao wakiwa ni wanawake na watoto – wamekimbia Syria, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa. Nchi jirani za Lebanon, Jordan na Uturuki zimeng'ang'ana kukabiliana na mojawapo ya uhamiaji mkubwa zaidi wa wakimbizi katika historia ya hivi karibuni.

Historia ndefu zaidi ya zama hizi imewekwa kwa kuzingirwa na kuchukuliwa tena eneo la mashariki ya Ghouta kutoka kwa uhalifu wa kivita dhidi ya ubinadamu uliochukua zaidi ya miaka mitano.
Takriban asilimia 85 ya Wasyria wanaishi katika umasikini, huku zaidi ya thuluthi mbili ya watu wakiwa ima ndani ya umasikini mbaya zaidi au uchochole. Zaidi ya watu 12.8 milioni nchini Syria wanahitaji usaidizi wa afya na zaidi ya milioni saba hawana usalama wa chakula huku kukiwa na ongezeko la bei na uhaba wa chakula. Familia hutumia hadi robo ya mapato yao kwa maji pekee. Baadhi ya watoto 1.75 milioni hawako shuleni.Na sasa kwa mara nyengine tena – hata wakati ambapo serikali ya Syria ilitumia silaha za kemikali kwa raia wake wenyewe, Umoja wa Mataifa ulishindwa kuleta mabadiliko kwa tatizo la watu wa Syria.

**Hitimisho**

Orodha ya nchi ambazo Umoja wa Mataifa imefeli kulinda raia wasio na hatia ni nyingi mno kuzieleza katika makala haya, huku Sudan, Afghanistan, Somalia, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Rwanda zikiwa baadhi yake tu. Umoja wa Mataifa uliundwa mnamo 1945 kama shirika la mwavuli wa kimataifa likiwa na malengo kadhaa msingi ikiwemo kuzuia vita na kudumisha amani katika maeneo ya mizozo. Lakini, mara nyingi Umoja wa Mataifa umefeli kote duniani zaidi kwa sababu haki ya turufu iko katika milki ya nchi tano pekee. zaidi umefeli katika ulimwengu wa Kiislamu kila wakati kwani umeundwa ili kuwapa hadhi ya juu wanachama wake wa kudumu wa Baraza la Usalama.

Na pindi Umoja wa Mataifa huu unapokuwa hautumikii maslahi yao, mataifa haya huenda kinyume na shirika hili – kama ilivyo fanya Amerika ilipoivamia Iraq mnamo 2003.

Hata wanapokuwa chini kama katika eneo la Srebrenica tunaona kuwa Umoja wa Mataifa haukuwa rafiki wa Waislamu, walisimama kando na kutazama mauwaji yakiendelea, licha ya kuwa wakaazi wa Srebrenica walikataa kuondoka, chini ya imani ya kimakosa kuwa majeshi ya Umoja wa Mataifa yatawalinda, lakini hawakuwasalimisha tu wanaume na wavulana wa Srebrenica bali pia waliwapa majeshi ya Serbia zaidi ya lita 30,000 za petrol ili kuwawezesha kuwasafirisha wanaume hao na kuwazika katika makaburi ya halaiki! Hivyo hivyo inaweza kusemwa kwa usaidizi wa uvamizi wa Palestina wa kimya cha bubu juu ya Burma.
Kuyaweka kwa maneno ya Balozi wa Amerika katika Umoja wa Mataifa, Nikki Haley, aliye zungumza mbele ya Baraza la Usalama juu ya Mashambulizi ya Kemikali nchini Syria alieleza: *"Pindi Umoja wa Mataifa unapofeli mara kwa mara katika jukumu lake la kutenda kwa ujumla, kuna nyakati katika uhai wa dola ambapo tunalazimika kuchukua hatua zetu wenyewe."*Sisi pia ni lazima tutambue kwamba tunahitaji kuchukua hatua yetu wenyewe kama Ummah. Na kufahamu kuwa tunaweza tu kutegemea usaidizi wa Mwenyezi Mungu (swt) pekee na kisha usaidizi wetu sisi kwa sisi. Kama alivyo teremsha Mwenyezi Mungu (swt):




[وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۚ إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُن فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ]

**"Na wale walio kufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipo fanya hivi itakuwako fitna katika nchi na fisadi kubwa."** [TMQ 8:73]. Ni Ummah huu pekee kiujumla ndio unaoweza kuzuia Srebrenica nyengine, kuikomboa Palestina na Kashmir na kumaliza vita nchini Yemen, na sio Umoja wa Mataifa. Hii yamaanisha ni lazima tuwashinikize watawala wa Waislamu na mujtamaa za Waislamu kuachana na nidhamu za utawala zinazotumikia Wamagharibi, na kuunda nidhamu ya utawala inayomtumikia Mwenyezi Mungu (swt).

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Office of Hizb ut Tahrir na**
**Yasmin Malik**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Misikiti itafunguliwa pasi na masharti na kulindwa na Khilafah na sio tawala za kisekula




Waislamu nchini Kenya na baadhi ya nchi duniani wamo katika tabu kutokana na misikiti yao kufungwa na tawala za kisekula kwa kisingizio cha kuwalinda Waislamu kutokamana na kuenea kwa janga la COVID-19 ndani ya sehemu za ibada. Kitendawili kilichopo nchini Kenya ni kwamba misikiti ilifungwa wakati ambapo idadi ya maambukizi ilikuwa takribani 100. Lakushangaza ni kuwa baada ya takribani miezi minne idadi imefikia zaidi ya 10,000+ na makadirio ya maambukizi kwa siku ya kiwa 200+ kwa maana yanaongezeka kila kukicha. Serikali ya Kenya mnamo 6 Julai, 2020 iliagiza lile linaloitwa Baraza la Dini Mseto linaloongozwa na Archbishop Anthony Muheria kutoa mwelekeo kuhusiana na hatua zitakazochukuliwa kwa maandalizi ya kufungua sehemu za ibada zinazojumuisha misikiti!

Hali hii imezifichua tawala za kisekula ambazo daima zinapiga njama dhidi ya Uislamu na Waislamu duniani kote. Haingii akilini kusikiza hoja na sababu zinazotolewa ili kuunga mkono kufungwa kwa misikiti ilhali kila mmoja anajua kuwa misikiti ndio vituo visafi na vyanzo vya kutafuta uokozi kunapotokea majanga katika jamii. Kufungwa kwa misikiti kumewafanya Waislamu duniani kuonja yale wanayohisi na kupitia ndugu zetu Waislamu kila umbile la Kiyahudi linapoweka vizuizi na kuvamia maeneo ya Qibla chetu kipenzi, Msikiti Al-Aqsa ili Waislamu wasiweze kuswali ndani yake pamoja na mashambulizi yake mapya ambapo mahakama ya Isreali imetoa uamuzi unaoagiza kufungwa kwa lango la Bab al-Rahma la Msikiti Al-Aqsa ndani ya Jerusalem Mashariki! (menafn.com, 14 Julai 2020). Kufungwa na kuharibiwa kwa zaidi ya misikiti 200 ndani ya Xinjiang na miji yake kujengwa upya ili kuwa sehemu za ujasusi kwa utawala wa Uchina. (bitterwinter.org, 20 Juni 2018) Nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) takribani misikiti yote 436 ili fungwa na kuharibiwa (www.ctvnews.ca, 17 Machi 2015)!

Hakika, Waislamu wanahitaji kwa dharura dola yao ya Kiislamu ya Khilafah ili kuwatunza na kuwasimamia mambo yao dunia kote. Ni hitajio la dharura ambalo ni lazima litimizwe kwa sababu inajulikana kwamba tawala za kisekula ni mabwana katika kupatiliza hali na hivyo wanaweza kupatiliza fursa ya hii ya kuwa njia panda ima kuendelea kufunga au kufungua misikiti nchini Kenya ili kuendeleza ajenda zao ovu za kuwabandikiza Waislamu kuwa wenye misimamo mikali au poa na hatimaye magaidi na kupelekea kutaabishwa zaidi!
Hatua ya kuchukua ni kutafuta suluhisho msingi kwa matatizo mengi yanayokumba Ummah wa Waislamu na dunia kwa ujumla katika kila nyanja ya maisha kuanzia kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu miongoni mwa mengine. Suluhisho msingi ambalo si jingine isipokuwa kusimamisha tena Khilafah ambayo imejaribiwa na kutawala kwa takribani karne 14 kwa huruma na kuwa msimamizi wa amani duniani. Khilafah itahakikisha kwamba sehemu za ibada zikijumuisha zile za raia wasiokuwa Waislamu ziko wazi na zinalindwa wakati wote. Maradhi yanapochipuza idara yake ya afya itahakikisha kuwa raia wote wamelindwa kutokamana na athari na ukali wa maradhi hayo na sera muafaka zitawekwa ili kuhakikisha kwamba maisha ya raia yanalindwa.

Kuchelewa kwetu katika kutafuta suluhisho la kudumu kumetupelekea katika hali yetu hii ya kuwa njia panda ya ima tufungue misikiti yetu kwa mujibu wa masharti ya serikali za kisekula au



kuendelea kuifunga! Njia zote hatimaye hazitatui tatizo. Hii inathibitisha kauli ya Mwenyezi Mungu (swt): وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا **“Na atakaye jiepusha na mawaidha Yangu basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki.”** [Ta Ha: 124] Na pia, Mtume (saw) aliizungumza hali hii: **لَيُنْقَضَنَّ عُرَى الْإِسْلَامِ عُرْوَةً عُرْوَةً فَكُلَّمَا انْتَقَضَتْ عُرْوَةٌ تَشَبَّثَ النَّاسُ بِالَّتِي تَلِيهَا وَأَوَّلُهُنَّ نَقْضًا الْحُكْمُ وَآخِرُهُنَّ الصَّلَاةُ “Mafundo ya Uislamu yatafunguliwa moja baada ya jingine, na kila fundo litakapofunguliwa litashikwa jingine, la kwanza kufunguliwa ni Utawala (Khilafah) wa Uislamu; na mwisho litakuwa ni Swala.” [Ahmad na Al-Hakim] Ni lazima tufanye haraka na tuunganishe juhudi zetu katika kuleta mfumo mbadala wa Kiislamu unaohitajika dharura ili kuchukua nafasi ya mfumo uliokufa wa kisekula wa kirasilimali. “«إِنَّمَا الإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ» “Kiongozi (Khalifah) ni ngao, nyuma yake mnapigana na kujilinda”**

**Ali Nassoro Ali**

**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahri**




# Usaliti Kwenye Ardhi Tukufu ya Bara Arabu

Tukiwa tumeingia ndani ya mwezi mtukufu wa Dhul-Hijjah tuna kumbushwa juu ya kujitoa muhanga kwa Kipenzi cha Mwenyezi Mungu, Ibrahim (as) alipomuwacha mwanawe na mke wake katika jangwa baina ya Safa na Marwa. Tunakumbuka kwamba miaka kadhaa baadaye Yeye na mwanawe Ismael (as) walijenga Al-Ka'bah. Tunakumbuka namna Ibrahim (as) alivyompiga Shetani na ni katika utiifu kwa Mwenyezi Mungu (swt) kuwa alikuwa tayari kumtoa muhanga mtoto wake bila kusita.

Ilikuwa ni katika ardhi hii hii tukufu ambayo ilishuhudia mapambano ya Haki na Batili katika Da'wah ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akiwakabili Maquresh. Alifanya Da'wah hadi alipopata Nusrah na kufanya Hijra Yathrib ambayo ikawa ndio dola ya mwanzo ya Kiislamu,

Mji wa dola ambao iliwatawala watu wake kwa yote aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu (swt). Haukupita muda mrefu dola hii ikaenea eneo lote la Hijaz na Najd na kufika Yemen kwa upande wa kusini na mipaka ya Sham kwa upande wa kaskazini. Ardhi hii iliobarikiwa imeshuhudia Ufunguzi wa Makkah (Fathi Makkah) na kuvunjwa kwa masanamu yaliowekwa ndani ya Kaaba. Imeshuhudia mwaka wa wajumbe ambapo makabila ya Arabuni yalijisalimisha kwenye Uislamu. Ardhi hii iliobarikiwa imekuwa na hadhi maalum, ambapo Dini mbili hazikubaliwi, kama ilivyopokewa katika kitabu cha Muwatta cha Imam Malik, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

«لاَ يَجْتَمِعُ دِينَانِ فِي جَزِيرَةِ الْعَرَبِ»

**"Hazichanganyiki dini mbili ndani ya Bara Arabu"**

Malik amesema kuwa Ibn Shihab amesema, “Umar ibn al-Khattab alitafiti juu ya habari hii hadi akapambanukiwa kwa uwazi kuwa Mtume (saw) amesema,

«لاَ يَجْتَمِعُ دِينَانِ فِي جَزِيرَةِ الْعَرَبِ»

"Hazichanganyiki dini mbili ndani ya Bara Arabu" Na hivyo akawafukuza Mayahudi kutoka Khaybar.”Kutokana na ujumbe wake SAW kumalizika kwa ushindi wa Uislamu, ardhi hii takatifu imeshuhudia kuondoka kwa mbora wa viumbe SAW, ikiwa ni huzuni kwa Ummah wake SAW. Ardhi hii takatifu imeshuhudia Mitume waongo alioangamizwa na Khalifah Abubakar as-Siddiq (ra). Ilishuhudia Khilafah Rashida, na kufuatiwa na utawala wa Kiislamu kwa karne nyingi. Ardhi takatifu imeshuhudia mapenzi ya Ummah na kuwajibika kwa Makhalifah katika kusimamia utawala wa Kiislamu juu yao.

Usaliti wa mwanzo ulishuhudiwa wakati Sharif Hussein na Ibn Saud wote wakishirikiana na Uingereza kwa ahadi ya kupata mamlaka juu ya ardhi hizi takatifu. Walikula njama dhidi ya Ummah na Dini na wakasaidia kuiangusha Khilafah ya Uthmani na hivyo kumaliza utawala wa Mwenyezi Mungu (swt) juu ya ardhi hii iliobarikiwa. Karne iliyopita ilishuhudia utiifu wa ufalme wa Saudia



kwa Uingereza na baadaye maslahi ya Amerika, kwa kipindi chote wakiinajisi ardhi iliobarikiwa kwa kutabikisha ukafiri. Utawala saliti uliruhusu vikosi vya Amerika kuingia katika ardhi hizi tukufu "kuikomboa" Kuwait mwaka 1991 na kuivamia Iraq 2003. Waovu (hao) wameendeleza vitisho kwa watu wa Yemen, ambapo vita vikiwa katika mwaka wake wa 6, vimewaacha watu wa Yemen wakiwa katika hali mbaya zaidi isiowahi kushuhudiwa.Kana kwamba haya hayatoshi, utawala wa Saudia umemkhini Mwenyezi Mungu kwa kuruhusu matamasha ya kipuuzi na uchafu wa wanamuziki wa kimagharibi na wachezaji densi kuwaharibu vijana.

Kama hili halitoshi mapema mwezi huu, Vogue Arabia iliandaa shughuli ya upigaji picha kwa wingi (photoshoot) iliyojumuisha wanamitindo wakuu mashuhuri wa kimataifa, wakionyesha uchafu jirani na msikiti mtukufu wa Madinah. Nini kingetarajiwa kutoka kwa wasaliti hawa waliozuia Hijja kwa Ummah wa Kiislamu, licha ya utajiri mkubwa na vifaa walivyonavyo? Wanaojiita Watumishi wa Misikiti Miwili Mitukufu hawawezi na hawataki kuwezesha utekelezwaji wa nguzo ya Uislamu isipokuwa tu kwa Mahujaji wachache wenyeji, lakini wamehiyari kuwezesha uchafu kwa jina la maendeleo.



Enyi Ummah uliobarikiwa wa Mtume aliyebarikiwa (saw), tunashuhudia usaliti huu juu ya ardhi hii iliobarikiwa na moyo wenu unachuruzika damu, lakini bado mumebaki kimya kwa usaliti huu. Kumbuka kwamba Mwenyezi Mungu ametupa sisi ushindi juu ya mataifa mengine.

[ كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ]

**"Nyinyi mmekuwa bora ya Ummah waliotolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu."** [Sura Al-Imran: 110].

Katika mwezi huu mtukufu ni lazima tutimize utukufu huu na jukumu hili. Na tutimize amri hii na tuwe sehemu ya chama kikubwa kabisa cha siasa cha Kiislamu ulimwenguni chenye kufanya kazi ya kuhuisha Dini ya Mwenyezi Mungu kupitia usimamishaji wa Khilafah, Hizb ut Tahrir. Sisi sote katika mwezi huu mtukufu tufanye kazi ya kusimamisha tena dola ya Khilafah kuwa miongoni mwa amali zetu njema kwa ajili ya Akhera yetu. Ni Khilafah pekee katika njia ya Utume itakayo safisha ardhi hii tukufu kutokana na uchafu wa ukafiri na kuikomboa na watu wake kutokana na wasaliti wanaotumikia Wamagharibi. Ni Khilafah ndio itakayoregesha Hijja katika njia yake ya sahihi na kukomesha ukandamizaji katika ardhi zilizobarikiwa za Sham na Yemen.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Maryam Ansari – Pakistan**




# 'YALIOTENDEKA' ZINGATIO TOSHA LA UMUHIMU WA FIKRA YA NDANI ILIYOKAMILIKA

Shabiki mmoja aliwahi kuandika katika kurasa ya facebook,'' ***We miss yaliyotendeka big. Infact we are no longer glued to Radio Citizen every day at 8pm as it used to be.''***

Kwa wapenzi wa radio hakika kifo cha Waweru Mbuga kitakuwa pigo kubwa mno kwani kitawakosesha kipindi sisimizi cha Yaliotendeka cha radio Citizen. Kipindi cha mwenda zake kiliwahi kuwa na wafuasi wengi huku wakivutiwa si tu na sauti yake bali kwa mada alizokuwa akizizungumzia.Mwenda zake Waweru Mbugu alikuwa kila siku katika kipindi hiki akichambua maswala ibuka yaliokuwa ni msiba kwa umma hivyo basi kufanya kipindi chake kuwa hai na muhali kusikiza.

Hamna shaka kusema kuwa kipindi cha yaliotendeka kilikuwa muhimu kwa jamii kwa kuwa kiliwahi kuweka na kujadili wazi masaibu ya jamii mbayo ni muhimu kujadiliwa.Muenda zake kwa kila siku kwenye kipindi baada ya kuanza kwa kusema,***''Hujambo msikilizaji, na karibu kwa yaliyotendeka..''*** alijaribu kwa kadri ya uwezo kutambuwa majanga ya jamii kwa kuyachambuwa uwovu wake na hata pia kuyatolea masuluhisho. Ndio,bwana Waweru Mbugu kupitia kipindi chake alikuwa gwiji wa kutambuwa na kubainisha majanga ya jamii lakini licha ya hivyo kipindi cha Yaliotendeka hakikuweza kuwapa jamii masuluhisho muafaka

Jambo hili si lakustaajabisha kwa kuwa yawezekana kwa mtu kuwa mtambuzi bora wa wakia lakini mtu huyu huyu akawa ni mwenye kushindwa kutambua suluhisha sahihi la wakia kama huo.Hivyo basi,mfano wa Mwenda zake na kipindi chake cha Yaliotendeka nikama mwanamuziki wa rege bwana Bob Nesta Marley.Itakumbukwa kuwa Bob marley aliwahi kuwa gwiji wa kutambuwa matatizo ya jamii huku akitumia ala ya muziki wa rege .Licha ya ugwiji wake wa utambuzi wa matatizo,vile vile pia nae aliwahi kushindwa kutoa masuluhisho muafaka.




Ama huwaje kukawa kwapatikana watu kuwa na uweza wa kutambua na kubainisha matatizo lakini kushindwa kutoa masuluhisho muafaka?Hili latokana na ukosefu wa fikra ya ndani kisha iliyokamilika.Ukosefu huu husababisha mja akawa ni mwenye kukosa kuunganisha mada yaani wakia[tatizo] na roho.Kufeli kwa kufungamanisha mada na roho hupelekea mja akawa ni mwenye kutumia akili yake iliyo na sifa ya kikomo,inayoathirika na mazingira isiyo juwa ghaib kuzua suluhisho ambalo kwa hakika simuafaka.

Hili tukilitilia maanani,kwa yule atakae endeleza kipindi cha Yaliotendeka au mfano wake,ili kuwezekane kupatikane muamko ulioshiba masuluhisho muafaka,hamna bundi kwa muendeshaji kipindi kujihami na fikra ya ndani iliokamilika.Laa sivyo jamii itahamasishwa tu kwa kupashwa matatizo pasi kuelezwa muelekeo wa kufuata.

ABU LEILA



# Maafisa wa Jeshi wachaMungu hupenda Jihad, wakitafuta Shahada au ushindi kwa ajili ya Radhi za Mwenyezi Mungu (swt)

Uislamu sio tu umefaradhisha Jihad pekee, umejenga hamu nzito ya Jihad ambayo imeutofautisha Ummah huu na mataifa mengine kwa karne kumi na tatu. Umeuwezesha Ummah huu kubeba hasara kubwa kwa hiari, ili kuwashinda maadui wa Uislamu na Waislamu. Kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu pekee, majeshi ya Waislamu yaliyashinda majeshi makubwa zaidi yaliyopigana kwa msingi wa imani fisidifu, ulinzi wa eneo au ubwana wa rangi ya ngozi. Kutimiza dori yao ya kuhakikisha Uislamu unatawala, majeshi ya Waislamu yaliondoa vizingiti vya kimada katika utabikishaji wa kivitendo wa Uislamu. Hivyo basi watu waliingia katika Uislamu makundi kwa makundi, na kuasisi misingi mipana ya Ummah wa leo, unaojumuisha matabaka ya rangi tofauti tofauti.

Hata baada ya kuvunjwa Khilafah mnamo 1924 M, mapenzi ya Jihad ndani ya Ummah huwahofisha maadui wa Waislamu. Miaka 25 ya kumbukumbu ya mauwaji ya Srebrenica yana mfano ndani yake. Huku takriban wanaume na wavulana wa Kiislamu 8,000 wa Bosnia wakiwa wameuwawa na Waserbia kwa kipindi cha siku kumi na moja, baada ya vikosi vya Kiholanzi vya Umoja wa Mataifa kuutelekeza mji wa Srebrenica mnamo 11 Julai 1995, Uingereza ilikuwa na wasiwasi kwamba vikosi vya Waislamu vilivyokuweko chini ya amri ya

Mapenzi ya Jihad yaliyoiporomosha Urusi ya Kisovieti hadi chini nchini Afghanistan, sasa yameilazimisha Amerika kuomba mpango wa kuokoa uso wake. Mapenzi ya Jihad katika Waislamu wa Kashmir Iliyokaliwa huihofisha Dola ya Kibaniani, ambayo imeiunganisha kwa nguvu Kashmir Iliyokaliwa mnamo 5 Agosti 2019, ilhali bado ingali inakumbana na upinzani mkali hadi leo.

Badala ya kukuuza mapenzi ya Jihad miongoni mwa majeshi, watawala wa Waislamu walioko sasa wanapigana kampeni kwa niaba ya dola za Kimagharibi na washirika wao, umbile la Kiyahudi na Dola ya Kibaniani, dhidi ya Kupingana katika njia ya Mwenyezi Mungu (swt). Ama watawala wa Pakistan, ni wachangamfu katika kudhoofisha hamu yenye harara ya Waislamu ndani ya jeshi la Pakistan ya kutangaza vita vya ukombozi wa Kashmir Iliyokaliwa. Badala ya kuwahamasisha maafisa wa Kiislamu na wanajeshi kupigana na kuikomboa Kashmir, wanawavunja moyo kutopigana na adui. Wanapigia debe fikra kwamba vita sio chaguo, ima kwa sababu ya adui kumiliki silaha za kinuklia au udhaifu wa uchumi wetu. Ama Waislamu watukufu wanaopigana dhidi ya uvamizi popote walipo, watawala wa kiimla wa Waislamu huwashutumu kuwa "magaidi". Lakini, kama ilivyo miradi yote ya mkoloni, jaribio hili la kuangamiza Jihad litafeli kwa sababu Ummah daima umeshikamana na

(saw) na kheri iliyoko ndani yake imeenea sehemu zote za mwili wake, ikiwemo majeshi yake.

Afisa wa jeshi aliye mtiifu kwa Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw) ni lazima aweke moyoni na akilini mwake kuwa Uislamu umeweka Jihad kama faradhi, ambayo kupuuzwa kwake kunakaribisha hasira za Mwenyezi Mungu (swt), huku kutekelezwa kwake huleta thawabu kubwa. Na azingatie yale yaliyotajwa kuhusu Jihad ndani ya Quran. Mwenyezi Mungu (swt) anasema,

[ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰ أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ]

**“Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui.” [Surah al-Baqarah: 216**



**Katika Ayah hii tukufu, Mwenyezi Mungu (swt) amewafaradhisha Waislamu walio na uwezo wa kupigana kutekeleza Jihad dhidi ya uovu wa adui anayefanya ufasiki dhidi ya Uislamu. Wakati huo huo Uislamu unatambua kwamba kupigana ni kitu ambacho kinasababisha upinzani ndani ya nafsi na kuutibu vilivyo upinzani huo. Mwenyezi Mungu (swt) anasema,**

**[وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ] "navyo vinachusha kwenu" ikimaanisha kuwa kupigana ni kugumu na kuzito nyoyoni. Hakika, kupigana ni kama Ayah ilivyo kusifia. Kunahusisha kuuliwa kama shahidi, kujeruhiwa, kupambana na maadui na kuvumilia uzito wa safari, ima katika baridi kali ya Siachen au joto kali la majangwa ya Thar. Mwenyezi Mungu (swt) kisha akasema, [وَعَسَى أَن تَكْرَهُواْ شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُم] "Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu" ikimaanisha, kupigana hufuatiwa na ushindi na tamkini juu ya adui.**



**Afisa wa jeshi Muislamu na azingatie yale yaliyotajwa kuhusu Jihad katika Sunnah. Utukufu wa Jihad ni maarufu ndani ya Sunnah ya RasulAllah (saw). Imepokewa katika Sahih,**

**«مَنْ مَاتَ وَلَمْ يَغْزُ وَلَمْ يُحَدِّثْ نَفْسَهُ بِالْغَزْوِ، مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّــة»**

**"Yeyote anayekufa na hakupigana (yaani katika njia ya Mwenyezi Mungu), na wala hakutamani nafsi yake kupigana, amekufa kifo cha kijahiliya (zama kabla ya Uislamu). " Katika siku ya ufunguzi (Al-Fath) (alipoifungua Makkah), Mtume (saw) alisema,**

**«لَا هِجْرَةَ بَعْدَ الْفَتْحِ وَلكِنْ جِهَادٌ وَنِيَّةٌ، وَإِذَا اسْتُنْفِرْتُمْ فَانْفِرُوا»**

**"Hakuna Hijrah (kuhama kutoka Makkah hadi Al-Madinah) baada ya ufunguzi, lakini Jihad na nia njema pekee. Mkitakikana mtoke, basi tokeni." [Bukhari] Mpokezi mkubwa wa Hadith, Az-Zuhri, anafafanua, "Jihad inahitajika kwa kila mtu, ima ajiunge kivitendo katika kupigana au abakie nyuma. Yeyote anaye bakia nyuma anahitajika kutoa usaidizi, endapo usaidizi utahitajika; kutoa msaada, endapo msaada utahitajika; na kusonga mbele, endapo ataamrishwa kufanya hivyo. Ikiwa hahitajiwi, basi atabakia nyuma."**

Hakika, Sunnah inawalingania Waislamu katika majeshi kwa lile ambalo ni lazima lipendwe, kupigana katika Njia Yake (swt), kutafuta ushindi au shahada ya juu kabisa. RasulAllah (saw) amesema,**«مَا أَحَدٌ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ يُحِبُّ أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا وَلَهُ مَا عَلَى الأَرْضِ مِنْ شَيْءٍ، إِلاَّ الشَّهِيدُ، يَتَمَنَّى أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا فَيُقْتَلَ عَشْرَ مَرَّاتٍ، لِمَا يَرَى مِنَ الْكَرَامَةِ»**

**“Hakuna yeyote atakaye ingia Peponi apende kurudi duniani hata alikuwa na kila kitu katika ardhi, isipokuwa Mujahid, atatamani arudi duniani auliwe mara kumi, kutokana na ile hadhi anayoiona (kutoka kwa Mwenyezi Mungu).”** [Bukhari]

**Afisa wa jeshi mwenye imani na azingatie kwamba kizazi cha kwanza na bora cha Uislamu kilitangaza Jihad ili kuwakomboa watu kutokana na watawala madhalimu, ili wauhisi Uislamu kivitendo.** Mwenyezi Mungu (swt) anasema,

[ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ قَاتِلُواْ الَّذِينَ يَلُونَكُم مِّنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ]

**“Enyi mlio amini! Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu, na wakute ugumu kwenu. Na jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wacha-Mungu.”** [Surah at-Tawbah 9: 123]. Mwenyezi Mungu (swt) anawaamrisha waumini, walio karibu zaidi na dola ya Kiislamu, kisha wale walio mbali zaidi. Hivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alianza kuwapiga vita washirikina katika Bara Arabu. Pindi Mwenyezi Mungu (swt) alipompa udhibiti juu ya Makkah,

Al-Madinah, At-Ta'if, Yemen, Yamamah, Hajr, Khaybar, Hadhramawt na mikoa mingine ya Kiarabu, na makabila mbali mbali ya Kiarabu kuingia katika Uislamu makundi kwa makundi, yeye (saw) alianzisha Jihad dhidi ya Watu wa Kitabu. Yeye (saw) alianza maandalizi ya kupigana na Warumi ambao eneo lao lilikuwa karibu zaidi na Bara Arabu, na kwa hivyo, walikuwa na haki kubwa zaidi ya kulinganiwa Uislamu. Hivyo, Mtume (saw) alikwenda hadi akafika Tabuk katika mwaka wa tisa baada ya Hijrah yake, akiuongoza Ummah katika kuzikabili dola zilizokuwa zikiongoza zama hizo.

Je, afisa mchaMungu wa jeshi atazingatia vitendo vya Makhalifah Waongofu *(Khulafaa Rashideen)* (ra), katika kuitekeleza kwao Jihad? Baada ya Mwenyezi Mungu (swt) kumchagulia Mtume (saw) Pepo Yake (swt), Khilafah kwa Njia ya Utume iliipa Jihad haki yake kamili. Khalifah wa Kwanza Muongofu, Abu Bakr As-Siddiq (ra), alianza kuyaandaa majeshi ya Kiislamu kupigana na Makruseda wa Kirumi na Majusi wa Kifursi. Kwa baraka ya misheni hii, Mwenyezi Mungu (swt) akamfungulia ardhi na kuleta udhalilifu kwa Kaisari na Kisra. Mikononi mwa Khalifah wa Pili Muongofu, 'Umar bin Al-Khattab (ra), Mwenyezi Mungu aliwadhalilisha makafiri, akafungua sehemu za mashariki na magharibi ya dunia kwa nuru ya utawala wa Kiislamu. Kisha, katika zama za Khalifah wa Tatu Muongofu 'Uthman (ra), ukweli usio na mithili wa Uislamu uliingia katika sehemu nyingi za dunia, ikiwemo bara dogo la India.



Na Khalifah wa Nne Muongofu, Ali (ra), alimakinisha udhibiti juu ya eneo linalojumuisha mabara matatu. Hivyo basi, Makhalifah Waongofu *(Khulafaa Rashideen)* (ra) waliuendeleza Uislamu, wakitoa ushuhuda katika maneno ya Mwenyezi Mungu (swt) [وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ]"Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wachaMungu." Afisa mtambuzi wa jeshi na azingatie kwamba pindi Jihad inapopuuzwa, maadui huwa na hamu ya kuzishambulia kambi za Uislamu, na kupata udhibiti juu ya ardhi nyingi za Kiislamu. Ilhali, kila mtawala mwadilifu wa Kiislamu au kamanda wa jeshi anapotimiza amri ya Jihad, Mwenyezi Mungu (swt) humpa nusra na kumfanya mshindi juu ya adui. Hakika, utekelezaji wa Jihad huleta utukufu, huku upuuzaji wake huleta udhalilifu. RasulAllah (saw) alitangaza, « مَا تَرَكَ قَوْمٌ الْجِهَادَ إلاّ ذُلّوا»

"Hakuna watu wowote wanaoiacha Jihad isipokuwa hudhalilika." [Ahmad]. Hivyo Waislamu walishindwa na Mongoli walipoipuuza Jihad na hatimaye wakawashinda kwa Jihad katika Ein Jaloot. Waislamu walioipuuza jihad walishindwa na Makruseda, hadi Salahudin alipowaongoza katika ushindi baada ya ushindi. Ama Khilafah Uthmani, iliendeleza Jihad kiasi ya kuwa miji mikuu ya Ulaya ikaanza kuanguka na ile ambayo ilikuwa bado haijachukuliwa ilitetemeka na kutetemeka.



Afisa wa jeshi anaye tafuta Jannah na azingatie hali ya Ummah hivi sasa. Kutoka katika yale yote yaliyoteremshwa na Mola wa Viumbe na historia ya watu wema na wale waliokuwa na mapungufu katika jukumu lao la Jihad, analazimika kusimama wapi?

Hakika tangu Ummah upoteze ngao yake, Khilafah, mnamo 1924, ulipoteza pamoja nayo Jihad ya kufungua ardhi mpya kwa Uislamu. Zaidi ya hayo, maadui walizikalia ardhi zake, ima iwe ni umbile la Kiyahudi linaloikalia Palestina upande wa magharibi au Dola ya Kibaniani inayoikalia Kashmir upande wa mashariki. Lakini, kunapokosekana Khilafah, kupigana na makafiri wanaozikalia ardhi zetu, hakusimami. RasuAllah (saw) amesema,

«وَالْجِهَادُ مَاضٍ مُنْذُ بَعَثَنِيَ اللَّهُ إِلَى أَنْ يُقَاتِلَ آخِرُ أُمَّتِي الدَّجَّالَ لاَ يُبْطِلُهُ جَوْرُ جَائِرٍ وَلاَ عَدْلُ عَادِلٍ، وَالإِيمَانُ بِالأَقْدَارِ»

**"Na Jihad imekuwepo tangu Mwenyezi Mungu aliponitumiliza hadi siku wa mwisho katika Ummah watakapopigana na Dajjal. Haibatilishwi na udhalimu wa dhalimu wala uadilifu wa mwadilifu, na imani juu ya Qadar."** [Abu Daud] Hivyo basi, kupigana na makafiri ni Faradhi, ima mtawala wa Waislamu awe ni Khalifah, au mtawala wa Waislamu awe hatawali kwa Uislamu. Kwa hayo, ni Faradhi juu ya majeshi ya Waislamu kuhamasika katika kupigana na majeshi vamizi. Endapo mtawala atakubali kupeleka jeshi, basi atakuwa amefanya sahihi. Endapo atajaribu kulizuia jeshi kutokana na kupigana, akawa

basi na kuwepo Salahuddin miongoni mwa jeshi hilo, atakayemkanyaga mtawala huyo chini ya miguu yake, na kuhamasisha jeshi kuzitakasa ardhi tukufu kutokana na uvamizi.Ni wazi kwamba watawala wa Waislamu walioko sasa ni kizingiti njiani mwa afisa wa jeshi huyu na utiifu wake kwa Mwenyezi Mungu (swt). Watawala wa Waislamu walioko sasa wanatangaza kuwa vita sio chaguo na kumtangaza yule anayepigana kama adui wa Ummah. Watawala hawa huwatesa wale wanaobeba silaha wenyewe ima dhidi ya Waamerika nchini Afghanistan au Dola ya Kibaniani katika eneo lilikokaliwa la Kashmir. Baya zaidi, wamesawazisha mahusiano na wavamizi, ambapo inamakinisha zaidi uvamizi wao. Hili ni hata ingawa Mwenyezi Mungu (swt) ameamrisha,

[وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُم مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ] **"Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni"** [Surah al-Baqarah 2: 191].

Ayah hii tukufu inatumika kwa wale wote wanaopigana na maadui wanaojishughulisha na kupigana na Uislamu na watu wake. Inamaanisha kwamba nishati yetu ni lazima itumiwe katika kupigana nao, kama ambavyo nishati yao inatumiwa katika kupigana na sisi, na katika kuwafurusha kutoka katika maeneo waliotufurusha. Hivyo, ni wazi kwa afisa huyu wa jeshi kwamba watawala walioko sasa kamwe hawatayafurusha majeshi vamizi kutoka katika Ardhi za Waislamu wala kurudisha Khilafah ili ufaradhi wa kufungua ardhi mpya kwa Uislamu uregee. Inamuangukia kila afisa wa jeshi kutibu hali hii mbaya. Kila afisa ni lazima asimame na Ummah na faradhi kubwa ya Jihad juu yao. Ni jukumu la maafisa wa jeshi kuwang'oa watawala walioko sasa, kunyosha Nusra yao kwa ajili ya kusimamisha tena Khilafah kwa Njia ya Utume (saw). Hapo na hapo pekee, ndipo watakapopigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu (swt), na kumaliza udhalimu kote ulimwenguni.



Hivyo, maafisa wa jeshi wa Kiislamu wa leo na wawe mithili ya Maanswari waliomnusuru Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume Wake (saw), kiasi ya kuwa Mwenyezi Mungu (swt) aliwasifu katika ayah Zake na malaika wakakimbilia katika mazishi ya bwana wao, Sa'ad bin Muadh (ra). Imepokewa na Tirmidh kutoka kwa Anas bin Malik (ra) kwamba RasulAllah (saw) alisema kuhusu mazishi ya Sa'ad bin Muadh (ra), «إِنَّ الْمَلَائِكَةَ كَانَتْ تَحْمِلُهُ» **"Hakika, Malaika walikuwa wanambeba."** Waliobarikiwa hakika ni wale maafisa wa jeshi wa leo wanaofuata njia ya Maanswari.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na Musab Umair – Pakistan**


O MUSLIM ARMIES
GAZA IS CALLING YOU!
HIZBUT TAHRIR MALAYSIA
DON'T KEEP CALM
START WORKING FOR KHILAFAH
MEMERLUKAN
DARI TENTERA UMAT

**Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari**

**REF: 1441 / 12AH**

# Chini ya kisingizio cha kupambana na COVID-19 kunafanywa bidaa mpya kwa Dini yetu

Serikali kupitia baraza la dini mseto (Inter- Faith) imefungua misikiti kwa mikakati mikali. Jopo hilo la wanachama kumi na tano lilipewa jukumu la kufanyakazi na wizara ya mambo ya ndani pamoja na wizara ya afya katika kuweka masharti ya kufunguliwa tena maabadi.Kati ya masharti hayo yanayopaswa kufuatwa kwenye nyumba za ibada ni; kuweka umbali wa masafa ya mita 1.5 baina wanaoswali, idadi ya watu 100 pekee kuruhusiwa kuabudu, watoto chini ya umri wa miaka 13 na watu wazima wenye umri wa miaka 58 kutoruhusiwa kuingia kufanya ibada na muda wa kufanya ibada usizidi saa moja.

Kwa haya, tungependa kueleza yafuatayo:

Fikra jumla ya maingiliano ya kiimani ni fikra ya kisekular isio na msingi wowote katika Uislamu.Hii ni kuwa fikra hii inatoa mwito wa kuweko na uiano baina ya imani mbalimbali za Kidini.Fikra hii aidha inalingia dini nyengine mpya kinyume na Uislamu ambayo Wamagharibi wanataka Waislamu wote kote duniani kuikubali dini hiyo. Binafsi wazo hili linalenga kuwafanya Waislamu waachane na mafundisho yao Kiislamu badali yake fikra za kisekular iwe ni kipimo cha Dini yao.

Sheria za Kiislamu zimetoka kwa MwenyeziMungu SWT (Wahyi),katu hazibadilishwa na mamlaka yoyote yale, tofauti na  kanuni za Kisekular zinazotokamana akili za mwanadamu hivyo huwekwa na kubadilishwa kulingana na mazingira. Na ndio kwa muktadha huu, twakumbusha masheikh ambao baadhi yao ni wanajopo wa baraza la Interfaith, walichotakikana ilikuwa ni kuweka bayana sheria za Kiislamu kuwa hazichukuliwi mahala popote pale ila kwenye machimbuko yake asili ambayo ni Quran, Sunna na Ijmaa na Qiyas.Hili ndilo jukumu la wanavyuoni wamchao Mungu nao hupaza kauli ya haki pasina kuogopa ya lawama ya mwenye kulaumu.

Utekelezwaji wa ibada ya Swala za Jamaa umeonyeshwa kivitendo na Mtume wetu Muhammad (Saw), hivyo si suala la kufanyiwa mashauriano. Kwa hali hii, ni faradhi kwa Waislamu wote kupanga safu wakiwa kwenye swalah pasina kuacha mwanya baina ya mtu mmoja na mwengine. Amepokea Almaalik Bin Al-huwairith Radhi za MwenyeziMungu zimshukie kwamba Mtume (Saw) alisema:

وَصَلُّوا كَمَا رَأَيْتُمُونِي أُصَلِّي وَإِذَا حَضَرَتِ الصَّلَاةُ فَلْيُؤَذِّنْ لَكُمْ أَحَدُكُمْ ثُمَّ لِيَؤُمَّكُمْ أَكْبَرُكُم

**Na swalini kama mlivyoniona nikiswali na inapowadia Swala, basi mmoja**

**wenu aadhini kisha yule mkubwa wenu kiumri aweze kuwaswalisha.**

Na akapokea Imam Ahmad kutoka kwa Abdullah Ibn Umar kuwa Mtume (Saw) alisema:

« أَقِيمُوا الصُّفُوفَ فَإِنَّمَا تَصُفُّونَ بِصُفُوفِ الْمَلَائِكَةِ وَحَاذُوا بَيْنَ الْمَنَاكِبِ وَسُدُّوا الْخَلَلَ وَلِينُوا فِي أَيْدِي إِخْوَانِكُمْ وَلَا تَذَرُوا فُرُجَاتٍ لِلشَّيْطَانِ وَمَنْ وَصَلَ صَفّاً وَصَلَهُ اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى وَمَنْ قَطَعَ صَفّاً قَطَعَهُ اللَّهُ»

**Simamisheni safu kwani safu zenu zinakua pamoja na za Malaika safu na muoanishe bega kwa bega, zibeni mianya na wafanyieni upole ndugu zenu na wala msiache mianya ya shetani. Atakayeunga safu MwenyeziMungu Naye atamuunga na mwenye kukata safu MwenyeziMungu naye atamkata.**

Ni bayana kutokana na dalili hizo hapo juu kwamba kuwalazimisha wenye kuswali kuweka umbali wa mita1.5, sawa iwe ni swala za Jumua ama za Jamaa kwa hofo ya maambukizi hasa ikiwa wale waumini hawana dalili kabisa za maambukizi kitendo hiki ni uzushi katika Uislamu. Fauka ya haya, maradhi ya maambukizi ni udhuru wa kisheria wa waislamu kutokwenda msikitini wala sio udhuru wa kuruhusu kuenda msikitini kisha kujiweka mita moja toka kwa mwengine wakati wa kuswali.

Kuhusiana na sharti ya kuruhusu watu 100 pekee kuingia msikitini, kuwazuia watu wazima wenye umri wa 58 na watoto chini ya umri wa miaka kumi na tatu,kitendo hiki sio kuwa hakigongani tu na mafundisho ya Kiislamu bali pia dhulma dhidi ya waumini Wakiislamu na ni jambo lisilomridhisha MwenyeziMungu SWT. Na mgongano mkubwa wa maadili ya uongozi kwa kuweka masharti magumu kwa wanaoswali ilhali barabarani, ofisini, maduka na maeneo mengine bado tunayaona yakifurika watu pasina masharti hayo ya umri.Je hii ina maanisha kwamba maradhi ya Covid-19 huweza tu kuambukizwa ndani ya Misikiti wala sio kwengineko na kwa hivyo ni lazima ifunguliwe kwa idadi maalumu ya waumini wenye umri maalum?!

Tunasisitiza kuwa janga hili ni changamoto na mtihani kutoka Muumba Aliyetukuka kwa waja wake ukitutaka kurudi Kwake Yeye kwa kwa kutubia na kunyenyekea kwa maamrisho yake. Kwa munasaba huu, kufunguliwa kwa misikiti kwa masharti magumu ambayo yanagongana na sheria za MwenyeziMungu kunafanya vifua vya vya Waislamu kuungulika kwa maumivu makali. Hata hivyo, tunafahamu kwa yakini kuwa kwa kusimamisha tena Khilafah kupitia njia ya Utume katika moja ya mataifa makubwa ya Kiislamu, Misikiti hivi karibuni itatukuzwa na Jina la MwenyeziMungu kutajwa ndani yake asubuhi na jioni.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**

# Jarida la UQAB



uqab.or.ke

uqab_htk

UQAB-Magazine-1911964012162253